# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**STRATHMORE HIGH SCHOOL**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

# STRATHMORE SCHOOL KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/1**

**KARATASI YA 1**

**INSHA**

**Mwongozo wa kusahihisha**

1. **Risala**

Hii ni insha ya Risala. Insha hii iwe na muundo ufuatao: -

i) Iwe na anwani ya mwandishi
ii) Iwe na mada ambayo itaandikwa kwa herufi kubwa na kupigiwa msitari
iii) Mtajo lazima uwepo
iv) Hitimisho iwe inaonyesha msimamo wa anayotuma Risala. Kisha ihitimishwe kwa jina la mwandishi na sahihi huandikwa. Pia cheo cha anayeandika.

Baadhi ya hoja ni: -

-Dini, wahubiri amani na utangamano wa kikabila
-Kuchagua viongozi waadilifu
-Kuhubiri umoja wa makabila
-Kuhimiza ndoa kati ya kabila mbalimbali
-Ugavi sawa wa rasilmali
-Kulinda mali asili za kabila mbalimbali

-Michezo katika makabila mbalimbali

- Kuhimiza uzalendo na utaifa
- Kuepukana na uongozi na viongozi wa kikabila
- Kuacha tamaduni zinazohubiri chuki/mgambo wa kikabila

Zozote 6 x 2 = 12
Muundo alama = 4
Lugha = 4
Jumla = 20

2. **SWALI LA PILI**

**Manufaa**

i) Tarakilishi itarahisisha ufunzaji wa masomo mbalimbali kwa upande wa mwalimu
ii) Itakuza na kuimarisha ubunifu miongoni mwa wanafunzi
iii) Hatua hii itamtanguliza mapema mwanafunzi katika ulimwengu wa tarakilishi na teknohama.
iv) Itasahihisha kuelewa haraka wa masomo kwa kurahisisha mada ngumu katika silibasi kwa mwanafunzi
v) Itaboresha matokeo ya mitihani kwa wanafunzi husika.
vi) Itaimarisha Uchumi wa watengenezaji wa tarakilishi na programu.
vii) Zitatumika katika utafiti
viii) Zitapunguza mzigo kwa wanafunzi wa kubeba vitabu vingi

**Hasara**

i) Ni ghali kutekeleza – itahitaji fedha nyingi
ii) Bila kuwepo kwa walimu walio na umilisi wa kutosha wa kompyuta, hatua hiyo haitakuwa na manufaa
iii) Kutakuwa na tatizo la usalama wa wanafunzi na tarakilishi zenyewe.
iv) Baadhi ya shule hazina miundo-msingi ya kutekeleza masomo kwa tarakilishi k.v. kawi na madarasa.
v) Zisipodhibitiwa, tarakilishi zitaweza kusababisha utovu wa maadili kwa wanafunzi kupitia mitandao

(hoja 5 katika kila upande)

**Tanbihi**
**-**Hii ni insha ya mjadala
**-**Iwe na upande wa kuunga na ule wa kupinga
**-**Katika hitimisho mwandishi aonyeshe msimamo wake

**3. Methali**

Mwanafunzi aandike kisa kitakacholenga maana ya methali hii kuwa anayekwenda nyuma na mbele ya jahazi huishia katikati ya chombo hicho. Hii ina maana kuwa enda uendako na kokote utakako lakini ukiwa bado u hai utarudi kwenu ulikotoka tu.

4.

- Hii ni insha ya mdokezo
- Lazima mwanafunzi aanze kwa maneno ya mdokezo
- Kisa kilenge mkasa wowote ule mfano:
- Uvamizi
- Kisa cha kujitoa uhai
- Ubakaji